

Mchango wa Wanawake wa Kiswahili katika Uongozi, Dini na Ushairi 1350 B.K-1840 B.K.

Kineene wa Mutiso
Chuo Kikuu Nairobi, Kenya

Ikisiri

Wataalamu wengi wa fasihi ya KiSwahili hawajui kwamba kuna washairi wengi wa KiSwahili wa kike, ambao wamechangia sana katika tasnia hii. Mshairi maarufu anayejulikana na wengi ni Mwana Kupona binti Mshamu. Ni wachache zaidi wanaojua hata kiongozi mmoja mashuhuri wa kike. Katika makala haya, nimeangalia mchango wa washairi na viongozi wa kike wa KiSwahili, wa upwa wa mwambao wa Afrika Mashariki na visiwani. Kwa kutoa ithibati za kimapisi na kiushairi, nathibitisha kwamba wanawake wa KiSwahili wamekuwa katika mstari wa mbele kiutunzi, kidini, kimapisi na kiuongozi, kwa muda mrefu sana. Wameshughulikia sio tu waadhi na mapenzi, mbali pia yale waandishi kwa kiume wa KiSwahili wameshughulikia. Nimejikita kati ya mwaka 1350 B.K na 1810 B.K. Nimeonyesha kwamba ni baada ya majilio ya watawala wa kigeni ambapo mwanamke wa KiSwahili alizidi kukandamizwa, kwa sababu za kidini, kitamaduni na kikoloni. Wa aidha, nimedhibitisha kwamba washairi na viongozi hawa wa kike walipatikana sio katika sehemu moja tu, bali katika upwa mzima na visiwani.

Maneno Muhimu: Wanawake, uongozi, dini, ushairi

Utangulizi

Katika fasihi simulizi na andishi za jamii mbalimbali duniani, mwanamke amesawiriwa na wanaume, na hata wanawake wenzake, kama kiumbe mwovu. Amesawiriwa kama anzali, bahili, chombo cha kuburudisha na kuzaa, goigoi, hasidi, laghai, kachero, malaya (ijapo hushirikiana na mwanamme katika kitendo hiki), majununi, mbishi, mchawi, mchimvi au maluuni, mchoyo, mdaku, mdukizi, mfitini, mjanja, mkwepuzi, mlaaniwa, mmbea, mkosa adabu, mnafiki, msaliti, mshari, mshaufu, mstareheshaji (hususa wa ngono), mtongozaji, mtoto, mtovu, mtundu, mwenye wivu, mzinifu, pambo, pumbazo, punda, safihi, sakubimbi, tunda, tapeli, ua, n.k (Wamutiso 2017a, 2014c, 2005a). Kwa sababu hii, ni lazima afundishwe adabu na kuongozwa, katika maisha yake yote. Umuhimu wake ni

katika kufanya kazi “ndogondogo” za nyumbani, kuzaa na kuwalea watoto tu. Akiwa kiongozi, hatarajiwi kuwa kiongozi mzuri na mwenye busara na akiwa mwandishi, jamii haitaraji aandike mambo ya maana, ila ya kawaida, kama ya kimapenzi na hususa ya kitoto!! Wanaume ndio viongozi na waamuzi katika takribani mambo yote. Ndio wazalishaji mali na ndio wenye uwezo wa kiuchumi. Kwa sababu hii, si ajabu kwamba wamewasawiri wanawake kwa dharau. Wanaume ndio wametunga vitabu vyta kidini, kimapisi, kisheria, kiisimu, makamusi, n.k. Hata katika fasihi ya ulimwengu mzima, hususa katika tenzi, si kawaida mwanamke kusawiriwa kama jagina, ila msaidizi wake na ghalibu ndiye humsaliti na kumwangamiza jagina. Hata hivyo, mwanamke amekuwa katika mstari wa mbele katika kujenga kila taifa duniani. Mchango wake katika kila jamii hauna kifani.

Kukandamizwa kwa mwanamke kumewafanya waandishi wengine wa kike duniani kutumia majina ya kiume, ili vitabu vyao vichapishwe na kuuzwa. Baadhi ya watanzi wa kike waliotumia majina ya kiume katika uandishi wao ni: Mtunzi maarufu wa kike kutoka Uingereza na mwandishi wa *visa vya Harry Potter*, Joanne Rowling au J.K. Rowling, ambaye alijiita Robert Galbraith; Mwingereza Mary Anne Evans, aliyejiita George Eliot; Ann Rule , aliyejiita Andy Stack; mtunzi Mmarekani, Louisa May Alcott, aliyejiita A.M. Barnard; mwandishi wa KiMarekani Alice Bradley Sheldon, aliyejitambulisha kama Tiptree; mwanariwaya maarufu na mtunzi wa *Jane Eyre*, Charlotte Bronte, aliyejitambulisha kama Currer Bell; mtunzi maarufu wa riwaya kama vile *Wuthering Heights*, Emily Bronte, aliyejiita Ellis Bell (pamoja na dada zake wawili waliotumia majina ya kiume), mwanariwaya marufu, wa kutoka Denmark na mtunzi wa *Out of Africa*, Karen Blixen, aliyejibatiza Isak Dinesen na Amantine Lucile Aurore Dupin, mzaliwa wa Paris, mwanariwaya maarufu, mhakiki na mtunzi wa *Indiana*, aliyejitambulisha kama George Sand.

Mwanamke wa KiSwahili, kama mwanamke wa jamii yo yote ile ulimwenguni, amewekwa nyuma. Yeye ni wa kuongozwa na kulindwa na mwanamume. Hata hivyo, wanawake wa KiSwahili, wametunga kazi muhimu, kama zile za wanaume. Wamekuwa MaSultana/WaFalme, MaSheha, MaChifu na MaJumbe/WaJumbe (sio kwa majina tu, lakini kwa vitendo), washairi na wanukuzi wa miswada maarufu. Kama tutakavyoona baadaye, WaSwahili walikuwa na hawa MaSultana si haba. Hata kiongozi mwanamke alipoitwa “Mwana” na jina hili kutarjumiwa kwa KiIngereza kama “queen”, jina halikumaanisha “mke wa mfalme”, bali “kiongozi wa kike anayeheshimiwa”, “Sultana” (Sultani), “Mfalme wa kike”, n.k. Viongozi hawa wa kike pia walikuwa wafanyibiashara maarufu. Viongozi na wafanyibiashara mashuhuri wa kike walipatikana katika miji ya kibiashara, kama vile Itsandra, Mombasa, Pate, Pemba na Zanzibar. Hata hivyo, uongozi wa wanawake, kama wa wanaume, ultofautiana, kutoka dola-mji hadi dola-mji. Na tukumbuke

kwamba wakoloni walieulewa utawala waWaAfrika kwa misingi ya utawala wao, lakini sio kwa misingi ya KiAfrika.

Wanawake wa KiSwahili waliongoza pasipo kuwa chini ya viongozi wa kiume. Habari kuhusu wanawake hawa hupatikana katika tarihi mbalimbali za WaSwahili, masimulizi ya mdomo, mapisi, mapisi-chimbo, shajara za kinasaba, kumbukumbu, miswada ya KiSwahili ambayo hupatikana katika maktaba za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, London, Berlin, Hamburg na katika barua zilizoandikwa katika karne ya kumi na sita ambazo zapatikana huko Goa, Bara Hindi. Ingawa katika makala haya nimerejelea kazi nyingi, katika kazi hizi, viongozi hawa wametajwa katika tanbihii za kazi tu. Ni wazi kwamba, ingawa mwanamke wa KiSwahili amegandamizwa toka zama za giza, WaArabu, WaShirazi, WaJerumani na WaIngereza walipokuja katika upwa wa Afrika Mashariki, mwanamke alizidi kukandamizwa. Sababu kubwa ilikuwa ni dini na tamaduni za watawala hawa. Utawala na dini za kigeni, ambazo zimejaa ubabedume, hazikumpa mwanamke nafasi ya kuendelea kutawala na kutangamana na mwanamme. Katika dini hizi za wakoloni, tunaelezwa ya kwamba mwanamke mmoja tu ndiye aliletu maovu takribani yote duniani. Kwa sababu amelaaniwa, hangeruhusiwa kuwa kiongozi. Ni kweli kwamba mwanamke, amekandamizwa kwa takribani kila dini na utamaduni, lakini katika dini na tamaduni zingine, kwa ujumla, amekandamizwa zaidi. Na si katika Afrika Mashariki tu, lakini katika uliwengu mzima, ambapo dini hizi na zingine, zimechangia pakubwa katika kuperomoka kwa uongozi wa kike. Viongozi wa kikoloni walipendelea kuwatumia wanaume katika uongozi wao. Jinsi dini na tawala za wageni hawa zilivoyzidi kuenea, ndivyo uongozi wa mwanamke ulivyoendelea kuperomoka.

Ingawa hatuna mengi ambayo yameandikwa kuwahuusu WaSwahili kabla ya kuja kwa wageni, tunaelezwa kuhusu viongozi wa WaSwahili, hata wa kike kama Mwana Mkisi wa Mvita, waliotawala kabla WaSwahili kusilimishwa. Mila za KiBantu zilimpa mwanamke mamlaka katika uongozi, mambo ya kijamii kama vile matambiko, uchumi, kufuata nasaba kukeni, n.k. Baadhi ya Waislamu waliokuja Afrika Mashariki, waliwaoa mabinti wa kifalme na kuwa masultani wenyewe. Kwa njia hii, uongozi wa kike ukapunguzwa. Hata hivyo, katika visiwa vya Komoro, uongozi wa kike uliendelea kwa muda, hata baada ya Uislamu na Ukristo kuenea katika sehemu hiyo.

Mwanamke wa KiSwahili anayejulikana sana na wataalamu wa KiSwahili ni Mwanakupona binti Msham (Werner/Hichens 1937, Damman 1940, Allen 1971, Knappert 1979, Khatib 1985, Njozi 1990, 1993; Biersteker 1991, Mulokozi 1995, Mulokozi na Sengo 1999; wa Mutiso 2003c, 2010; Maawy 2011), n.k.

Masultana wa Kike Us wahilini

Katika sehemu hii nimejadili masultana wa kike katika jamii ya Us wahilini. Masultana hao wamegawika ifuatavyo: Masultana wa Visiwa vya Tanzania na Komoro; Masultana wa Mombasa; Masultana wa Pate, Takwa, Witu na Visiwa Vya Wabajuni.

Masultana wa Visiwa vya Tanzania na Komoro

Katika upwa mzima wa Afrika Mashariki (pamoja na visiwa vyake, visiwa vya Komoro na Bukini vikiwemo), kumekuwa na viongozi wa kike sitini na wawili (62, Amirell 2015). Idadi ijulikanyo ya viongozi wa kike wa Us wahilini (visiwa vya Komoro vikiemo) ni ishirini na watano (25). Katika visiwa vya Komoro kulikuwa na viongozi wa aina hii kumi na tisa (19) na Bukini kumi na sita (*khj*)¹

Katika mswada mmoja wa KiSwahili (MS 380654a), “Swahili letters from Goa”, ambao uko School of Oriental and African Studies (SOAS), kuna mswada mmoja ulioandikwa kwa mkono. Mswada huu ni mkusanyiko wa barua ambazo zimeandikwa kwa KiReno na KiSwahili na kwa hati ya KiSwarabu (hati ya KiArabu iliyotumiwa/itumiwayo katika maandishi ya KiSwahili). Ni mojawapo ya nakala ya miswada ya hifadhi za barua au nyaraka za Goa, ambayo inahusiana na utawala wa KiReno katika Mwambao wa Afrika Mashariki. Mojawapo ya barua hizi imeandikwa kwa hati za KiSwarabu na Sultana Fatuma/Fatimah bin Mohammed/Muhammad (takribani karne ya 18), sultana, mfalme wa kike au kiongozi wa Kilwa KiSiwani. Fatuma bin Muhammed, aliomwandikia Mwinyi Jumaa, Mwenyeji wa Mvita au Mombasa, ambaye alikuwa Goa wakati huo. Barua hii inaanza kwa maneno yafuatayo: “Bismillahi ar-Rahmani ar-Rahim, mimi mfalme wa Kilwa Sultani Fatima ibnati...”. Sultana Fatima/Fatuma bin Mohammed alizandiika barua kwa KiSwahili cha zamani cha Kusini ambacho pia ni KiNgozi takribani karne ya 18 (takribani 1215 A.H). Yumkini wakati huu, KiNgozi ndicho kilichozungumzwa katika upwa mzima na visiwani.

Katika mapisi na tarihi, tunaelezwa kwa kifupi sana kwamba kulikuwa na viongozi wa kike katika upwa wa Pwani ya Afrika Mashariki na katika visiwa vyake. Viongozi hao walikuwa wa huko Luziwa, Mafia, Mikindani, Mombasa, Ngazija, Ngumi, Pate, Pemba, Siyu, Takwa (Manda), Tumbatu, Witu, Zanzibar, n.k. Mikindani ni mji wenye bandari, wa zamani na wa kibashara wa Tanzania Kusini, Kaskazini mwa upwa wa Msumbiji. Wakazi wake wa mwanzo walikuwa ni WaMakonde. Katika karne ya tisa (9) wafanyakazi wa KiArabu waliingia mji

¹ Kama hapo juu, keshatajwa. Vifupisho vinginge ambavyo nimevimetumika katika kazi hii ni kama vile *nw*, na wengine.

huu. Katika karne ya kumi na saba (17), wakati wa utawala wa Sayyid Said, kikundi kikinge cha WaArabu kikaingia mji huu. Misikiti na makaburi ya wakati huo, bado huonekana. Katika karne ya kumi na saba (17), wakati wa utawala wa Sayyid Said, kikundi kikinge cha WaArabu kikaingia mji huu. Misikiti na makaburi ya wakati huo, bado huonekana.

Katika karne ya kumi na saba Miji-dola ilikuwa ni Lamu, Lindi, Mafia, Malindi, Mombasa, Mtwara, Ngazija, Pate, Pemba, Siyu, Tongoni, Tumbatu, Vumba, Witu, Yumbwa, Zanzibari, n.k. Mikindani ni mji wenye bandari, wa zamani na wa kibiashara wa Tanzania Kusini, Kaskazini mwa upwa wa Msumbiji. Wakazi wake wa mwanzo walikuwa ni WaMakonde. Katika karne ya tisa (9), wafanyakazi wa KiArabu waliingia katika mji huu.

Kuna viongozi wa kike wa Zanzibar, kama vile Mwana Fatuma binti Ali (mwanzoni mwa miaka ya 1800/yumkini 1845, (Gray, 1960; Prins, 1961; Askew 1999; na Ingrams 1931/1967). Katika masimulizi ya WaZanzibari, viongozi wa Zanzibar pia wameorodheshwa kama viongozi wa Tumbatu na Hadimu. Mathalani, tunaelezwa ya kwamba Fatumah binti Ali alikuwa ni kiongozi wa kisiwa cha Tumbatu tu.

Yeye alifutwa na Mwana Kazija binti Ngwali (mwanzomwanzo wa 1800/au mwanzomwanzo wa 1900, Gray, 1960; Gray, 1961; Prins, 1961; Ingrams, 1931/1967, na Askew, 1999), naye akafuatwa na Mwana Miveni (Pouwels, 1987), ambaye alifuatwa na Mwana wa Mwana (miaka ya mwanzomwanzo wa 1800/ au katikati ya 1900, Bennet, 1978; Gray, 1960; Prins, 1961; Mathew 1956 na Askew, 1999). Mwana wa Mwana aliolewa na Hasan II bin Ahmed. Pia kuna kijisiwa kinacho julkana kama Mwana, karibu na kisiwa cha Tumbatu, kilichopo Kaskazini mwa Unguja. Mwana wa Mwana (Mana Vamoana) ndiye alikuwa mfalme au Sheha wa kike wa mwisho wa WaTumbatu. Katika masimulizi, tunaelezwa kwamba alipoolewa na mfalme Mwenyi Mkuu au “Mfalme” wa WaHadimu, Hasan II bin Ahmed, aliyeaga 1845, mjukuu wa Mwana Fatuma binti Yusuf, WaTumbatu hawakutozwa kodi tena na WaUmani. Isitoshe, kuna madai kwamba pepo aitwaye Gongoni binti Gongoni anatokana na ukoo wa Mwana wa Mwana. Mwana wa Mwana alifuatwa na Sheha, mwanawe Ali bin Hassan, naye akafuatwa na Fatuma ambaye alifuatwa na Vuai bin Mkadamu, ambaye alifuatwa na binamuye, Mwana Kazija binti Ngwali/Ngwale bin Kombo bin Ali (mwanzoni mwa miaka ya karne ya kumi na tisa), ambaye alifuatwa na ndugu yake Ali (Ingrams, 1931/1967)). Utawala tukufu wa Tumbatu unaishia hapa. Kuna kiongozi wa kike (miaka ya 1560), ambaye hatajwi kwa jina, lakini alitawala Cambo. Kulingana na kumbukumbu za KiReno na masimulizi ya WaSwahili, katika mwaka wa 1569, gavana wa Monomotapa, Francis Bareto, alimtembelea mwanamke huyu (Gray 1960, 1961).

Aidha, WaHadimu, ambao wako Kaskazini mwa kisiwa cha Zanzibar walikuwa na MaSultana kama vile Mwana Aziza (Pouwels 1987, 1891/1959; Gray 1960) na Mwana Mwema (takribani miaka ya 1650; Gray, 1960, 1962, 1977, Bennett, 1978; Prins, 1961; Strandes, 1961; Ingrams, 1931; Askew, 1999 na Stigand, 1966).

Katika shairi moja katika *Diwani ya Muyaka*, Muyaka anamrejelea Mwana Aziza akisema:

T'umwi ukifika Zinji, Zinji la Mwana Aziza (Abdulaziz 1979:130-131).

Mwana Mwema (karne ya17), alikuwa ni Sheha, Sultana au Malkia wa WaHadimu/Watumbatu (Bennett 1978:12, Gray 1961:129; 1962:51, 83, 159-160; 1977:138; Prins 1961:97). Makamu wake alikuwa ni Waziri Mkuu na chini ya Waziri Mkuu kulikuwa na afisa aliyejulikana kama makata. Aliolewa na Hassan, Mwenyi Mkuu. Pia aliwahi kuolewa na Mwarabu wa KiUmani na alikuwa na mtoto aitwaye Abdullah. Katika mwaka 1652, wakati watawala wa KiYarubi wa Umani, huko Zanzibar, waliishambulia ngome ya WaReno. Mwana Mwema aliwaasi WaReno na kuwa katika upande WaUmani. WaReno waliwashinda WaUmani kivita na kuuangamiza mji wa Mwana Mwema. Baada ya muda mfupi, WaUmani walilipiza kisasi na kuushambulia mji wa Mombasa, kati ya 1696 na 1698. Inasemekana kwamba ndugu wa kiume wa mumewe, Hassan bin Ali aliongoza baada yake. Katika masimulizi mengine ya WaZanzibari, nduguye Mwana Mwema, Yusufu, alishikilia au yumkini aliongoza kwa muda mfupi (Gray, 1977; Prins, 1961). Kuna wale wasemao kwamba aliyeongoza ni Fatumah, miaka ya 1690-1720 au kati ya 1696-1710 (Gray, 1962 na 1977) au (1697– takribani 1728, Askew 1999). Fatumah alikuwa ni mjukuu wake Mwana Mwema. Katika masimulizi mengine, Mwana Fatumah alikuwa mwanawewe Hassan bin Ali na ndiye aliyeongoza baada ya babake. Yusufu alichukua uongozi baada ya Mwana Fatuma binti Yusuf kuhamishwa huko Umani, kwa sababu ya kujaribu kuwasawaidia WaReno huko Mombasa, kati ya 1696 na 1698. WaReno waliwashinda WaUmani na Fatumah akahamishwa huko Umani kati ya 1700 na 1709. Baadaye, aliruhusiwa kurudi nyumbani. Katika masimulizi mengine, Fatumah hakuwasaliti WaReno, yumkini kwa sababu alikumbuka vile WaReno walivyomfanyia Mwana Mwema. Baada ya kurudi, katika mwaka wa 1710, Fatumah aliruhusiwa kuishi katika mji wa Zanzibar. Katika mwaka 1697, Fatumah alimwandikia barua gavana, ambaye alikuwa Goa wakati huo. Fatumah ndiye kiongozi wa kike wa mwisho wa WaHadimu, ambaye habari zake zimehifadhiwa, kimaandishi. Mumewe alikuwa wa ukoo wa Alawi, kutoka Hadhramaut, na aliwahi kuwa kiongozi wa Utondwe. Yeye na Abdullah, mfalme wa Otondo/Utondwe, walipata mtoto wa kiume aitwaye Hasan bin Abdullah, ambaye katika masimulizi mengine ya WaZanzibari, aliridhi utawala baada ya mama yake. Hassan aliwahi kuishi na mamake uhamishoni (Umani). Katika masimulizi mengine, baada ya Mwana Fatumah, mpwa wake Vuai bin

Mkadamu, ndiye aliwaongoza WaHadimu. Vuai alifuatwa na Mwana Kazija bint Ngwale bin Kombo bin Ali naye akafuatwa na nduguye, Ali (karne ya 17, Gray 1960, Askew 1999 na Abdulaziz 1975).

Kulingana na masimulizi ya WaSwahili na pia kumbukumbu za KiReno, kuna viongozi maarufu wa Pemba kama vile Mwana Hadiya/Mwana Hidaya (karne ya 17, Gray 1960, Askew 1999:102), Mwana Fatma binti Darhash(karne ya 17, Gray 1960, Askew 1999), Mwana Aisha (karne ya 17, Gray 1960, Askew 1999) na mwanamke asiyejulikana jina (takribani 1680, Gray 1960, 1969; Strandes 1961 na Askew 1999) na ambaye kufikia mwaka 1686 alikuwa amebatizwa na kuwa Mkristo na kuwapatia WaReno nchi yake. Kulikuwa Mwana Maryamu wa Yumbwa (Pouwels 1987) na kiongozi mwingine wa kike, ambaye hatajwi kwa jina, wa Luziwa (Prins 1961) na Mwana Sabani binti Ngumi wa Mikindani (miaka ya 1880, Gray 1960 na Askew 1999). Mmoja wa wazazi wake alikuwa Mswahili na mwingine Mmakonde na bintiye alichukua uongozi baadaye) wa Mikindani. Viongozi wengine wa kike ni Mwana Shambi Shale/Mwana Chambi Chandi Ivor/Mana Chamby wa Vumba/Umba/Vumba kuu, Mwana Kazija na Mwana Nguya wa Kizimkazi na Mwana Fatuma wa Vumba (Nicholls 1971).

Huko Kua, katika kisiwa cha Mafia, kulikuwa na viongozi kama vile Mwana Mwanzuani/Anzuani (mwanzomwanzo wa 1800/mwishomwisho wa karne ya 18, Saadi 1941, Freeman-Grenville 1975 na Askew 1999) na mamake Mwana Mwanzuani, ambaye hatajwi jina lake. Mamake Mwana Mwanzuani/Anzuani (mwishomwisho wa 1700), alikuwa ni Mshirazi. Kulingana na masimulizi ya WaMafia, Mwarabu mmoja, kwa jina Aidarusi, alisafiri hadi Kua na kukutana na kiongozi huyu wa kike, ambaye hajulikani jina, na kumwoa binti yake, Mwana Anzuani. Baada ya kuolewa, Mwana Anzuani aliendelea kuishi Kua, hata mumewe aliporudi Hadhraaut, ambapo alifia baadaye (Freeman-Grenville 1975; Saadi 1941).

Wanawake wengi walitawala katika visiwa vya Ngazija: Sultana wa kwanza kutawala nchi ya Ngazija, kama vile Said Bakari bin Sultani Ahmed Ngazija (Harris 1977) anavyotueleza, ni binti Kunie, ambaye alitawala Bajini, halafu Bara binti Jataru, Nemanya Ikvaba (Hambu), Nyao Fauine (Itsandra), Alimah II, mfalme wa Anzuani (takribani 1632 – takribani 1651, Stewart 1999); Alimah III, Mfalme wa Anzuani (takribani 1676- takribani 1711, Stewart 1999), Djambaba binti Djumbamba wa Bajini, Komoro (takribani 1880, Truhart 2002), Djana Niema binti Djumbe Fumu wa M'Budi, Komoro (takribani 1880, Truhart 2002), M'Zade M'Ba-Jini wa Bajini, Komoro (takribani 1880, Truhart 2002), Barwedja N'Draru wa Bajini, Komoro (takribani 1873–1880, Truhart 2002), Singa wa Madi wa M'Budi, Komoro (takribani 1850–1860, Truhart 2002), Jumbe Fatimah wa Mohéli, Komoro (1842–1868, Stewart 1999), Djumbe wa Halima III binti Muhammad, Hamahame, Komoro (1803–1803, Truhart 2002), Djana Fena,

Bajini, Komoro (takribani 1814– takribani 1836, Truhart 2002:1064), Halimah wa Anzuani, Komoro (takribani 1788– takribani 1792, Stewart 1999), Monavo Fani wa Mayotte, Komoro (takribani 1714–takribani 1720, Stewart 1999), Wabedja Seha la Djumbe wa Itsandra, Komoro (?–1743, Damir *n.w.* 1985), Nema Feda wa Hamahame, Komoro (?–1743, Damir *n.w.* 1985:55), Ais(h)a wa Mayotte, Komoro (takribani 1700–takribani 1714, Stewart 1999:157) na Wabedja, Sultanah wa Itsandra, Ngazidja (Komoro Kuu), aliyetawala nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa (19). Alihimiza maendeleo ya kibiashara, ikiwa ni katika kuyaendeleza yale yaliyokuwa yameanzishwa na mwanawe (Damir *n.w.* 1985:57).

Masultana wa Mombasa

Katika tarihi na masimulizi ya zamani ya Mombasa na kuhusu viongozi wa kike katika pwani ya Afrika Mashariki, tunaelezwa ya kwamba Mwana Mkisi ndiye mtawala wa kwanza, takribani 1500 B.K. Ndiye mwanzilishi wa mji wa kifalme wa Kongowea au Gongwa (Mombasa). Hii ndio sababu ya mji wa Mombasa kuitwa Mji wa Mwana Mkisi. Aidha, ndiye mtawala wa kwanza wa kike na asiye Mwislamu wa Mombasa, kabla ya kuwasili kwa Shee Mvita, ambaye pia hujulikana kama Shehe Mvita wa Msham, Shahu (mfalme au manju) Mvita, Shahu/Shaha Mushaham(u), Shahu M(i)sham, ibn Hishām, Ibn Misham na Shahu/Shaha (mfalme) Mahasham. Masimulizi ya WaSwahili na ya WaReno yana maelezo kwamba baadhi ya viongozi wa miji ya WaSwahili, kuanzia karne ya kumi na sita na hata baadaye, walikuwa ni wa kike. Hata hivyo, habari kumhusu Mwana Mkisi hazipatikani katika masimulizi ya WaShirazi, yanayohusu mapisi ya Mombasa. Shehe Mvita (930-1000 A.H /1515-1592 B.K), ndiye anatajwa kama mwanzilishi wa Mombasa, katika masimulizi hayo (Berg 1968a:42-44; Hichens 1938b:3-33; Taylor 1924:80-83, Pouwels 1987:218, Strobel 1979:76).

Inasemekana kwamba mji wa Mwana Mkisi ulikuwa karibu na Hospitali kuu ya sasa ya Kaunti ya Mombasa, upande wa magharibi mwa daraja inayounganisha kisiwa na bara. Mji huu ulienea hadi katika eneo linalojulikana kama Bondeni.

Katika ubeti ufuatao tunaona vile Mwana Mkizi anavyohusishwa na ushujaa:

Gongwa la Mwana Mkisi, kwamba wataka lingia

Kaageni wenu mbasi, wake na watumba goya

Muje kwa p'epo za kusi, mupate kuangukia

Ngoma ya kizungup 'ia, Wagongwa waipigile

(Abdulaziz 1979:12 na 132).

Mombasa ni mji wa Mwana Mkisi, kama mwataka kuingia huko (kuushambulia)

Mkawaageni marafiki, wanawake na wapenzi wenu
Mje kwa pepo za Kusini, ili mweze kufika pwaa
WaMvita wajua kuicheza vyema, ngoma ya vita (fasiri yangu)

Mji huu ultawaliwa na Mwana Mkisi, lakini baadaye Uislamu uliletwe na WaShirazi, ambao baadaye waligombana naye. WaShirazi walinyakua uongozi wa kifalme na kumpatia Shehe Mvita. Katika masimulizi na katika kazi zingine za kimapisi, za Mombasa, tunaelezwa kwamba Mwana Mkisi alimwachia uongozi mwanamume mmoja wa KiShirazi, Shehe Mvita. Nilipowahoji baadhi ya wazee wa KiSwahili, huko pwani ya Kenya, walidai ya kwamba Shehe Mvita alikuwa ni Kiongozi wa kidini na Mwana Mkisi alikuwa kiongozi wa kisiasa.

Aidha, inasemekana kwamba Kongowe a ulikuwa ndio mji wa Mwana Mkisi na Mvita ndio ulikuwa mji wa Shehe Mvita. Hii ndio sababu mji huu akauita au ukaitwa Mvita. Hata hivyo, Mvita pia ni mji uliojukana kama Kongowe, Mji wa Kale, Gongwa na Mji wa Mwana Mkisi. Muyaka wa Muhaji ameurejerea mji huu kwa majina haya yote. Sehemu ambayo Shehe Mvita alitawala ilisilimishwa takribani kati ya ya karne ya kumi na tatu (13) na kumi na nne (14). Jambo hili linadhibitishwa na Ibn Battūta katika mwaka wa 1331 B.K. Mji wa KiShirazi ulikuwa Kusini Mashariki mwa Kongowe. Hata hivyo, mchakato wa usilimishaji ulikatizwa kwa muda katika karne ya kumi na sita (16) na kumi na saba (17), kufuatia uharibifu wa Mvita uliofanywa na WaReno na vilevile uhamaji wa WaKristo ambao hawakutaka kusimilimishwa kule Gavani. Hata hivyo, mji wa Mvita ulipata wakazi wapya na kuitwa Mji wa Kale. Mchakato huo, wa kusimilishwa, ultokea tena baada ya serikali ya WaReno kupinduliwa na WaArabu, baada ya 1698 B.K.

Katika masimulizi mengine, MwIslamu wa kwanza Mombasa ni Shehe Mvita (Berg na Walter 1968b:53, SOAS ms 373394a, faili, 373394, “The Mombasa Chronicle” 1317 A.H/1899). Tarihi ya Mvita (The Mombasa Chronicle) ilitungwa na kunakiliwa, kwa hati za KiRumi, na Khamis bin Sa’id bin Shaikh al-Mambasi. Shehe Mvita wa Msham alikuwa pia ni mshairi wa Mji wa Kale, yaani Mvita (mji wa Shehe wa Mvita) na mwanzilishi wa uongozi wa kifalme wa kwanza wa KiIslamu na wa KiShirazi, mjini Mombasa. Nduguye alikuwa ni Shehe Ahmed bin Abubakr bin Salim al-Jaufy. Shehe Mvita aligombana na al-Jaufy, na al-Jaaufy pamoja na wafuasi wake, wakatoka Mvita na kuwa waanzilishi wa Junda. Inasemekana kwamba Shehe Mvita alitoka Ushirazi na majahazi yake na kushukia Kisau, ambapo alijenga mji na akaishi hapo pamoja na watu wake. Ukoo wa utawala wa KiShirazi ultawala Mombasa kati ya 1590-1730 B.K. Shehe huyu anakumbukwa kama MwIslamu aliyekuwa mwanachuoni maarufu na kwa sababu hii, anahuishwa na mafundisho ya sasa ya utamaduni wa WaSwahili. Mataifa Tisa ya WaSwahili, ambayo hujikana kam “Thenashara Taifa”, yamehifadhi mapisi, mila na desturi za kiasili za WaSwahili. Ingawa kwa

sasa Mombasa ni mji wenye utamaduni mseto, familia ambazo zinahusishwa na Mataifa Tisa bado huchukuliwa kuwa wakazi wa kwanza wa mji huo.

Freeman-Grenville (1962), akirejerea mwanamapisi ambaye halitaji jina lake, anasema kwamba Shehe Mvita wa Msham ndiye kiongozi wa KiShirazi aliyetawala Mombasa, wakati WaReno walipotamalaki kisiwa hiki katika karne ya 16. Uongozi wake wa kinasaba wa KiShirazi uliondolewa na utawala wa kinasaba wa KiShirazi wa Malindi. Shehe Mvita aliondolewa madarakani na WaReno, kwa sababu aliunganisha WaKilifi na WaMvita dhidi yao. Wakati WaMvita na WaKilifi walipopigana na WaReno, WaReno walileta WaSegeju, kutoka Malindi, na kuwashinda, walimwondoa Shahwa Mvita uongozini.

Katika masimulizi mengine, tunaelezwa kwamba ni baada ya kifo chake, ambapo WaReno walimteua Ahmad bin Hassan al-Malindi (wa Malindi) kuchukua nafasi yake. Kulinga na masimilizi haya, Shehe Mvita alifia Mvita, wakati huo wa utawala wa WaReno na hata kaburi lake liko Mombasa, katika Mash'had abayo huitwa "kwa Shehe Mvita".

Masultana wa Pate, Takwa, Witu, Visiwa Vya Wabajuni

WaPate nao walikuwa na MaSultana wao kama vile Mwana Khadija binti Omari/ Mwana Khadija binti Bwana Tamu ndogo/Mwana Mimi au Mwana Khadija bint Bwana Mkuu bin Abubakar bin Muhammad bin Abubakar bin Muhammad bin Abubakar bin Muhammad bin Umar bin Muhammad bin Ahmad bin Muhammad bin Seleman au Mwana Mimi Bwana Tamu Mkuu (1769-1776 au 1764-1773/4, Nicholls 1971, Freeman-Grenville 1975, Stigand 1966, Tolmacheva 1993, Truhart 2002:627 na Askew 1999:102) na dadake Fumo Luti, mwanamke wa kwanza kuwa Sultana wa Pate. Katika masimulizi ya WaPate na katika miswada mingine, Mwan Khadija alikuwa ni Sultana wa Witu tu.

Mwana Khadija alikuwa ni binamu wa hayatı Sultan Bwana Tamu Mtoto, Sultan wa Pate takribani 1160 – 1177 A.H (1745 – 1768/1747-1764). Alifanyiwa fitina nyingi na WaPate, hata ikafikia wakati mmoja akawa anatawala wakati mmoja na Sultan Umar. Alipigana na Sultan Umar kwa miaka mitano hata Sultan Umar akakimbilia Barawa. Baadaye, Sultan Umar alipata nguvu na kurejea Pate, lakini usiku akauliwa na watu wa Khadijah (Werner 1914/5:285-288). Sultana mwingine wa Pate (na Siyu) alikuwa ni Mwana Masuru/Musura wa Pate/Siyu (Pouwels 1987, Nurse na Spear 1985, Gray 1960, Taylor 1924, Sacleux 1941 na Tolmacheva 1993:66-68, 76-77, 177, 180, 231-236, 260-265, 304-308, 353-356, 398-402, 445-49). Alikuwa na watumwa na alimwachilia mmoja wao alipogundua kwamba aliweza kupiga/kupuliza pembe.

Kuna madai kwamba Mwana Masuru/Musura alikuwa Msanye na kwamba kulikuwa na Mbatawi mmoja ambaye wakati mmoja alikwenda kununua pembe

za ndovu kutoka kwa Mwana Masuru na baadaye akamwoa bintiye. Hata kuna wimbo unaouhusu kisa hiki:

Pate nda Mwana Masuru, Pate ni ya Mwana Masuru

Akizanya pembe akitwaa na ushuru, alipouza pembe alitoza ushuru pia

Kuna MaSultana wengine wa Pate kama vile Mwana Fatumah binti Darhast (karne ya 17, Gray, 1961:121) na Mwana Darini binti Bwana Mkuu bin Abu Bakar (takribani 1670-takribani 1700, Nicholls 1971 na Askew 1999:102, Tolmacheva 1993:66-68, 76-77, 177, 180, 231-236, 260-265, 304-308, 353-356, 398-402, 445-49).

Huko Takwa/Kitao, katika kisiwa cha Manda, alitawala Mwana Inali (karne ya 17, Stigand 1966, Pouwells 1987 na Askew 1999:102). Sultana huyu alijitosa baharini kutoka kilele cha mlima wa Kitao/Takwa, wakati ambapo alisikia kuwa wazee wa Kitao/Takwa walikuwa wameenda kwa Umar, huko Pate, kutaka amani (Stigand 1966:42).

Mwana Mtama alikuwa ni Sultana wa Witu.

Kuna wanawake ambao wasifu wao umeandikwa katika minbar ya makaburi yaliyo katika Afrika Mashariki (Freeman-Grenville/Martin 1973:102-122). Baadhi ya habari hizi hazipatikani katika mavza za Afrika Mashariki, lakini katika Makumbusho ya fur Völkerkunde, huko Berlin. Baadhi ya wanawake hawa ni kama vile Sayyida ‘Ā’isha bint Mawlānā Amīr ‘Alī b. Mawlānā Sultān Sulaymān, aliyeaga dunia 761 A.H/1359-60 B.K au 961A.H/1553-4 B.K.(katika makumbusho ya fur Völkerkunde), Mwana (Miyān) b. Mwana Madi b. Mwana Sa’īd al-Malindānī, aliyeaga 24 Muḥarram 1124/3 /A.H. Machi, 1712. Awali wasifu huu wa marehemu, Mwana (Miyān), ulikuwa katika minbari ya msikiti wa Malindi ya Kilwa Kisiwani, lakini sasa uko katika Makumbusho ya fur Völkerkunde, Berlin. Wengine ni ‘Ā’isha bint ‘Alī al-Hātam (? al- Hātim) b. Ḥabīb (aliyeaga Shawwal 625 A.H/17 Septemba 1228 B.K (katika minbari ya KiIslamu msikiti wa Mogadishu), Fāṭima bint ’Abd al-Samad b. Yāqūt, aliyeaga 23 Jumāda al- Ūlā, 7 1300 (minbari ya KiIslamu ya msikiti wa Mogadishu) na Hājjīya Bibi bint Muqaddam Hājj Muḥammad, aliyeaga 5 Dhūl-Ḥijja [I]138/4 A.H/1726 (minbari ya KiIslamu ya msikiti wa Mogadishu). Kuna wasifu wa marehemu Mwana wa Bwana binti Mwidani, aliyeaga 29 Rajab, 866/29 A.H/Aprili, 1462 B.K (katika mibari ya KiIslamu ya Tuaka, karibu na Kilindini, Mombasa), wasifu wa marehemu Mwana Mājid bint Ma’ādī b. Wabi al-Kindīya, aliyeaga 5 Ramadhān 1207/16 A.H/Aprili, 1793 B.K), Mwana Siti bint Diwan Hasan, aliyezaliwa 23 Rabi’l, 1162/14 A.H/ Marchi 1749 B.K (katika minbari ya msikiti wa Vumba) na wasifu wa marehemu Sayyida ‘Ā’isha bint Mawlānā Amīr ‘Alī b. Mawlānā Sultān Sulaymān, aliyeaga 761A.H/1359-60 B.K au 961 A.H/1553-4 B.K (katika minbari ya msikiti wa Kilwa Kisiwani).

Majina ya wanawake wasifika yamepatikana katika minbari ya misikiti ya Kenya (Faza, Gazi, Gedi, Jumba la Mtwana, Kinuni, Lamu, Malindi, Mambrui, Mnarani, Mtwapa, Muungi, Mwana (Ras Mwana), Ngome ya Isa, Pate, Siu, Takwa, Wasini, n.k), Tanzania (Bagamoyo, Bweni Kuu, Chole, Dar es Salaam, Kaole, Kigomeni, Kilwa Kisiwani, Kiomoni, Kipumbwe Mji Mkuu, Kunduchi, Mafia, Marungu, Mboamaji, Mbweni, Ndumi, Songo Songo, Tanga, Tongoni pa Mtang'ata, Ukutani, Ushongo Mtoni, Utondwe, n.k), Visiwa vy'a Komoro (Domoni, Anzuani, n.k) na Somalia (Barawa, Mogadishu, Bargal, Chovai, Laso 'Arro, Makunbusho ya Garesa, Marka/Merca, n.k).

Asha binti Muhammad, Asha Ngumi au Mwana Ngumi, maarufu kwa jina Asha Ngumi (karne ya 13? – takribani 1686), alikuwa sio Malkia tu, bali Sultana wa kisiwa kidogo cha WaBajuni kiiwtachoo Ngumi. Kiongozi huyu alihodhi na kutawala kisiwa hiki na sehemu yote kutoka kisiwa hiki hadi Shungwaya, sehemu iliyojulikana kama Ford Durnford. Alikuwa maarufu kwa kuwa wa kwanza kuwapatia Wagarreh madini ya chuma. Wakati huu, WaGarreh walikuwa wakiishi Deshek Wama na walikuwa hawajui matumizi ya madini haya. Madini ya chuma yalitumiwa kutengeneza mikuki ya chuma, ambazo ndizo ziliwuwa silaha mpya, zilizochukua nafasi ya silaha zilizotengenezwa kutohana na pembe choroa, ambazo ziliwuwa zikiwekwa kwenye mawano ya mikuki.

Wakati huu wa utawala wa Asha Ngumi, takribani mwaka 1686, kiongozi mwanamume, aliyejulikana kama Kisisi, alishika usukani lakini hakuwa maarufu kama Asha Ngumi. Kiongozi huyu alikuwa ni kiongozi wa kabilia la Punun au Pulun na alikuwa katili mno. Alikuwa akivunja ubikira wa biarusi kwa kumtoboa kwa kidole kikubwa cha mguu. Jambo hili lilimghadhishwa chifu Borali bin Mwii, chifu wa kabilia la WaBorgau na adui mkubwa wa chifu Kisisi. Chifu Borali bin Mwii, pamoja na wafuasi wake, walimjulisha Asha Ngumi, kuhusu tabia ya unyama ya Kisisi. Asha Ngumi aliwajulisha machifu wa WaGarreh, huko Deshek Wama. Yeye na machifu hawa walipanga kumsaidia Borali kwa kila hali na kikosi chake cha WaArabu ili kumpiga vita Kisisi na WaPunun wote. Asha Ngumi alikuwa jagina kweli. Akiwa na kikosi cha askari elfu moja (1,000) na kwa kushirikiana na wa machifu wa WaGarreh, walimgwangamiza Kisisi na Borali akatawala tena, kama awali (Elliot 1925/26: 10-22 na 147-163, 254, 354-355, Askew 1999:102). Kulingana na Allen (1993:143-144), Punun alikuwa ni kiongozi mdogo katika sehemu ya Shungwaya, ambaye alipata uongozi mkuu kwa njia isiyofaa. Allen (*khj*) anasema kwamba Punun ndiye alikuwa akiwatoboa mabibi arusi bikira. Kisa hiki kuhusu Punun, hupatikana katika masimulizi ya WaSiyu, WaDigo na WaSegeju, ingawa kuna tofauti ndogondogo hapa na pale.

Kulingana na Elliot (1926b: 354-355), takribani mwaka wa 1700 B.K, wimbo/shairi lifuatalo lilitungwa, kumhusu Kisisi:

*Tulia na Fuma, Tulia na Fuma,
Ngumi na Koyama Ngumi na Koyama,
'Pana kiwa tena hakuna kisiwa (kingine) tena
Sikisahauni ! Ah! Msikisahahu!*

II

*Kiwa cha Shungwaya - Kisiwa cha Shungwaya
Vaume talaiya wanaume shambulieni
Valifuma taiya waliwafuma (waliwaua) mahayawani
(Kwa muvi moiya) (kwa mshale mmoja),
Usishi ngweni mingine ikibaki mkononi*

III

*Uvucha mbwa mungauta uta ni wa mnga
Ngwe nda mkongwa ngwe ni ya mkongwa
Mabele nda kanga mishale ni ya kanga (ina mabele ya kanga)
Maeka kitwani matumizi yake kichwani (ni kazi ya kiongozi)*

IV

*Thicha nda kitayi vita ni dhidi ya hayawani
Mabele nda chayi mishale ni ya tai
Nani vafumayi? ni nani wafumaji (ataogopa?)
Fumanu rerevu! fumeni (piganeni) kishujaa
Tulia na Fuma, Tulia na Fuma
Ngumi na Koyama Ngumi na Koyama
'Pana kiwa tena hapana kisiwa tena (hakuna kisiwa kingine)
Sikisahauni! Msisahau*

II

*Kiwa cha Shungwaya Kisiwa cha Shungwaya
Vaume talaiya wanaume (majagina) shambulieni
Valifuma taiya walifuma (waliua) mahayawani
(Kwa muvi mmoya) (kwa mshale mmoja)
Usishi ngweni mingine ikibaki mkononi*

III

*Uvucha bwamunga uta ni wa munga
Ngwe nda mkongwa ngwe ni ya ufumwele/mkono stadi
Mabele nda kanga,mishale ni ya kanga (iliyo na manyoya ya kanga)
Maeka kitwani, mikakati (yao pamoja) ni kichwani (kazi ya kiongozi)*

IV

*Thicha nda kitayi, vita ni vya hayawani
Mabele nda chayi, na mishale ina manyoya ya tai
Nani vafumayi? nani kati yenu ni wafumaji ?
Fumanzi rerevu! fumeni (piganeni) kishujaa(fasiri yangu)*

Tulia ni kisiwa ambacho hivi leo huitwa Buli, Kaskazini mwa Fuma. Wimbo huu ni juu ya Chifu Kisisi, wa Wapununi, kiongozi ambaye nimemweleza hapo juu, kiongozi ambaye nimemweleza hapo juu, aliyeangamizwa na askari elfu moja (1,000) wa mfalme Mwana Ngumi/Asha binti Muhammad/Asha Ngumi, wakishirikiana na askari wa Borali bin Mwii (chifu wa WaBorgau na adui mkubwa wa Kisisi) na wa machifu wa WaGarrreh. Maana ya ubeti wa kwanza ni kwamba njama za kumwua kiongozi Kisisi zilitokana na wakazi wa visiwa hivi vinne - Fuma, Tulia, Ngumi na Koyama. Hakuna mwingine alihusika katika njama hizi. Shungwaya inaitwa “kisiwa”, kwa sababu sehemu moja imezungukwa na hori na sehemu nyingine vinamasi vya mikoko, ambavyo hufurika wakati wa bamvua.

Maana ya ubeti wa pili ni kwamba askari waliopigana na Kisisi ni mashujaa wa kivita. Hayawani anayetajwa katika mshororo wa kwanza, ubeti wan nne, ni Kisisi, ambaye aliwfanyia wanawake unyama. Asha alikuwa si Sultana tu bali kiongozi mwenye uwezo mkubwa sana na aliongoza sio katika kisiwa chake tubali hadi Port Dunford (Shungwaya).

Washairi wa Kike wa Kiswahili

Kabla kuja kwa WaReno katika Afrika Mashariki, Sultani Omar aliitamalaki Manda katika mwaka wa 750 A.H/1350 B.K. Ndiye alikuwa kiongozi wa kwanza kuwatoza raia wake kodi ya *kikanda*, ambayo ilikuwa ni pauni 180, kwa kila kikundi cha watumwa (Stigand 1913:43-44). Sultani Omar aliwapeleka mateka wa kisiwa cha Manda katika kisiwa chake cha Pate, ambako walishurutishwa kujenga ukuta uliokizinguka kisiwa hicho. Sehemu iliyozungukwa na ukuta huu iliitwa “weng’andu/wangandu”, yaani sehemu ya matajiri wavaao ng’andu (dhahabu). Mwanamke mmoja wa Kisiwa cha Manda alikataa kubeba mawe ya kuujenga ukuta wa Kisiwa cha Pate. Asikari akampiga, naye akaanza kulia. Mwanamke mwenzake, kutoka Kisiwa cha Manda pia, naye akamtuliza kwa kumwomba aache kulia. Katika wimbo/shairi hili ambalo alilitunga mwaka (750 A.H/ tarehe 9 Julai 1350 B.K.), huyu mwanamke wa kutoka kisiwa cha Manda, anamkumbusha mwenzake kwamba walipokuwa kwao Manda, viongozi wao waliwatesa watu, kama vile walivyokuwa wakiteswa wakati huo (wakiwa mateka Pate):

*Tuli kwetu Manda Tulipokuwa kwetu nyumbani Manda,
Twalitukitenda Tulikuwa tukiyatenda (kuwafanyia wengine maovu),
Yeo tukitendwa Leo ni sisi tunatendewa (tunafanyiwa maovu)*

*Twakataa kwani? Kwa nini tukatae (kufanyiwa maovu)?
Mwatupa ukuta Mwatuspatia ukuta tuujenge
Watupetapeta Ambao unatupetapeta/hutufanya tuchoke tukizunguka kisiwa (kwa kujenga ukuta wa kukizunguka kisiwa)
Kutwa in kuteta Kila siku hubishana,
Hatuna usono Hatuna mapumuziko (raha).*

Mwana Khamis Mwinyi Mvita (Karne Ya 16/1631)

Machache mno yanajulikana kuhusu Mwana Khamis Mwinyi Mwita. Mtunzi huyu alizaliwa na kukulia Mombasa na aliishi katika kipindi cha utawala wa WaReno. Alitunga wimbo/shairi “Mzungu Migeli” lifuatalo:

*Mzungu migeli u muongo Wewe Mzungu (Mreno) Miguel ni mwongo (umekosea)
Mato yako yana tongo macho yako yana matongo (na kwa huwezi kuona vizuri)
Kwani kuata mpango Kwa nini umeacha mpango?
Kwenda kibanga uani? wako kuvunja ahadi? (tafsiri yangu)*

Kulingana na Chiraghdin (1974:5), Mwana Khamis Mwinyi Mvita alitunga wimbo /shairi hili katika mwaka wa 1631. Hichens (1963:123), anadai ni katika mwaka wa 1660 na Taylor (1924:95-96) anasema ya kwamba lilitungwa baada ya WaReno kuhama Mombasa

Mshairi anamtahadharisha kasisi wa KiReno, Miguel, ambaye ni rafiki yake, kuhusu kisengo (mauaji makubwa). ambacho kitarajiwa kufanyika. Inasemekana kwamba mwanzoni, WaReno waliishi vyema na WaSwahili, wenyeji wa mjni Mombasa, lakini baadaye wakaanza kuwatumia vibaya na hata kuwanyanya baadhi yao. Waliwashika kwa nguvu wanawake wa KiSwahili na kuwafanya hawara zao. Vitendo hivi vilisababisha kisengo kikubwa. Wakati huu, kulingana na Taylor (*khj*), kulikuwa na Mreno mmoja ambaye inasemekana kwamba alikuwa kasisi. Kasisi huyu alikuwa na mwao mzuri na wakazi wa mji huo (wa WaSwahili), hata akajifunza na kuijua vizuri lahaja yao (KiMvita). Wakati WaSwahili walipopanga kuwasenga WaReno, watu wengi walikubaliana, shingo upande, kuwa ingefaa kumwangamiza kasisi huyu, pamoja na WaReno wenzake.

Habari hizo ziligunduliwa na bikizee, ambaye aliamua kumwokoa kasisi huyo. Alitunga wimbo ambao nimeutaja hapo juu, akamwita kijakazi wake na kumwimbia wimbo/shairi hilo mara kadha. Akamwamuru kwenda kuuimba wimbo huo tena nje ya nyumba alimokuwa akiishi Miguel peke yake na akamwambia: “ lazima uendelee kuuimba hadi atakapokwambia uache kuimba”. Kijakazi huyo akafanya namna alivyoamrishwa. Mzungu Miguel alipohisi kulikuwa na jambo ambalo halikuwa la kawaida katika uimbaji huo, akaandika chini maneno hayo na kuyachunguza kwa makini. Mwishowe, alipokisia maana yake, hakupoteza muda wo wote, bali alienda kwenye ngome (ya Isa) na akafanya

mashauriano na wanajeshi wa KiReno. Akawashauri wawe waangalifu na wasiende kwa karamu waliyokuwa wakiazimia kusheherekeea mashambani kesho yake.

Hata hivyo, kwa kuwa hangeweza kutoa sababu yoyote mwafaka ya ushauri wake, isipokuwa wimbo huu hapo juu, onyo lake lilipuziliwa. Siku iliyofuatia, wakati wanajeshi walipokuwa wakirejea kutoka kwa karamu yao vijijini, ambako walikuwa wamekunywa pombe kali zaidi ya mnazi, na kulewa chakari chordo, chupa na kizibo chake, walivamiwa ghafla bin fuu. Wengi wao waliuliwa njiani, wakielekea ngomeni. Miguel, aliyekuwa amebakia mjini, pamoja na wale wanajeshi waliofanikiwa kurudi, wakatorokea njia ndogo sana ambayo hata magofu yake huonekana hadi sasa. Wakaelekea katika meli iliyokuwa imetia nanga nje ya bandari.

Maoni haya ya Taylor (*khj*), yanaoana na kisa kimoja cha WaSwahili. Kulingana na Morris na Snoxall (1965:30-34), WaSwahili wana hadithi ifuatayo kuhusu Migeli (Miguel):

Zamani, WaReno walipotawala Mvita, palikuwa Mzungu mmoja Mreno, jina lake Migeli. Mzungu huyu hakukaa na wenzake bomani mwao, bali alikaa mjini. Alikuwa mtu mwema, akapendwa sana na wenyeji wa nchi. Wakati ule, wenyeji wakafanya shauri la kuwaua Wareno wote, kwa sababu Wareno waliwatendea vibaya, wakawasumbua sana wakawaiba binti zao. Tena, wenyeji wakafikiri ya kuwa ajapokuwa Migeli alipendwa sana, lakini lazima auawe pamoja na Wazungu wengine. Lakini rafiki yake mmoja mwanamke mzee aliposikia hivi, alifanya hila amponye Migeli. Akatuma kwake kijakazi mmoja, akimwambia, “Utakapofika kwa Migeli uimbe wimbo huu hata atakapokukomesha”.

Mzungu Migeli yu mwongo.

Macho yake yana chongo.

Kwani kuacha mpango

Kwenda kibanda uani

Chanzo cha picha hii na itakayofuta hapa chini ni Morris na Snoxall (1965).



Basi kijakazi yule akafanya kama alivyoambiwa, akafika kwa Migeli, akaimba wimbo ule mara nyingi. Migeli aliposikia maneno hayo alifikiri sana, halafu akakisia maana yake.

Migeli alipotambua maana ya wimbo wa kijakazi aliondoka kwake, akaenda mbio bomani, akawaambia askari za Kireno, akawaonya, “ Leo msiente nje; mkienda nje mtauawa na wenyeji”. Lakini askari hawakufahamu maneno yake, wakacheka tu. Asubuhi askari wakaenda wote kucheza michezo mjini, na walipokwisha kucheza wakanywa divai, na wengine wakalewa. Walipokuwa wakirudi bomani, wenyeji wengi wakawashambulia, wakaua askari wengi. Wale waliookoka wakakimbia, wakarudi bomani Migeli alimokuwa amekaa, wakafunga upesi, vyombo vyao. Wakaondoka, wakashika njia iliyopita chini katika bomba, wakafika ngome ndogo iliyoitwa Serani. Walipofika pale waliona merikebu bandarini (Kilindini), wakapanda merikebuni, wakatweka matanga, wakaenda zao pamoja na Migeli. Wakati huu hakubaki Mreno hata mmoja Mvita; lakini miaka mingi ilipopita, Wareno walirudi tena, wakawashambulia wenyeji, wakautawala tena mji na nchi yake.

Shairi hili pia linaweza kuwa ni kejeli ya Mwana Mvita kwa WaReno. Mshairi, Mwana Mvita, katika beti mbili hapo juu, yumkini anawashambulia WaReno (ambao ni MaNasara au Wakristo) kwa ujanja na upofu wao (upofu wa macho na wa roho). Wana macho lakini hawawezi kuona ukweli katika *Kur'ani Tukufu* au yale wanayoyaamini WaIslamu. Hawawezi kutengemewa, kwa sababu ni waongo na ni walevi.



Melamps. G Morris '31.

Mwana Mwarabu Binti Shekhe Mwana Lemba (Karne Ya 17):

Siri la Asirali/ Utendi wa Andharuni/ Anzaruni

Wanawake, kama wanaume, walikuwa na wangali walimu wa mapisi, fasihi na utamaduni wa KiIslamu, kwa jumla. Mojawapo ya tenzi za KiSwahili za zamani zaidi ni *Utenzi wa Siri li Asirali*, uliotungwa na Mwana Mwarabu Binti Sheikh Bwana Lemba, katika mwaka wa 1074 A.H /1663 B.K. *Siri li Asirali* ndiyo kazi ya kwanza, inayojulikana, ambayo imetungwa na mwanamke. Kuna miswada kadha katika makataba ya SOAS na katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mathalani, katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuna miswada nambari 305 uk. 1-37, 307 uk. 67 -75, n.k . Utenzi huu una beti 563 (mishororo 2,252) na kuna miswada mingine ambayo ina beti 562 (mishororo 2,248) na 557 (mishororo 2, 228). Muswada mmoja ulinakiliwa, kwa hati za KiRumi na marehemu Pera Ridhwani wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam. Muswada mwingine wenye beti 563 ulichapishwa na Ernst Dammann (1940) katika *Dichtungen in der Lamu Mundart des Suaheli Band*. Niliutarjumi na kuuhakiki kwa mara ya kwanza kwa KiIngereza, pamoja kutoa maelezo yake (2003b) na nikauhakiki tena kwa KiSwahili (2010).

Utenzi huu mkongwe unahusu nguvu za hirizi. Hirizi hii ya Anzaruni (Andharuni, katika KiTikuu), iitwayo *Siri li Asirali* au *Siri ya Siri zote , Siri Sirini*, au “Mwujiza wa Miujiza yote”, iliaminika kuwa na nguvu za kipekee. Ina majina tisini na tisa ya Allah na kwa sababu hiin ni aina ya sala. Anayesali akiwa na hirizi hii, hupatiwa chochote ambacho huomba, hata kama akiomba milima au mbingu ipotee kabisa!! Kwa sababu ya uzito wake, elimu iliyofichika ndani yake, nguvu za ajabu na baraka nyingi za hirizi hii, ni malaika 70,000 walioweza kuibeba (ubeti wa 449). Hirizi hii ina faida nyingi kushinda *Sefu li-kati'ati*, “upanga ukatao”. Ni kubwa mara kumi kuliko mbingu na ardhi (ubeti 458) na ajuaye

majina yote yaliyo katika hirizi hii ana baraka za Allah katika maisha yake yote. Ndiyo chanzo za nguvu zote duniani na hakuna kitu kizuri na chenyе manufaa zaidi kama hirizi hii. Anayeipata hirizi hii hatapatwa na dhiki yoyote na akifa hataonana na malaika wa kifo; Munkar na Nakir. Hataeswa kaburini asilani, kwa sababu Allah amemlinda kutokana na kuteseka. Hirizi hii ni dawa ya magonjwa yote.

Ni hirizi yenye mafumbo na siri ambayo Allah peke yake ndiye ajuaye maana yake. Katika hirizi hii, majina yote tisini na tisa ya Allah yameandikwa kwa wino tofauti tofauti wa dhahabu na wa kuvutia, kutoka Hijaz. Inabeba majina ya siri ya Allah na ye yote anayeyamiliki na kuyafahamu majina haya, Allah yuko naye. Hata kama ni kafiri, Allah pia humlinda milele na hakumbwi na hatari yoyote kila mahali aendapo. Hirizi hii humkinga anayeimiliki dhidi ya hasira au ghadhabu za Allah na ujanja/hila za wanadamu. Pia humkinga ye yote anayeibeba au kuivaa dhidi ya kifo, ugonjwa na uharibifu. Pia huwapa watu wema utulivu wa akili na utoshelevu.

Katika utenzi huu, tunaelezwa kwamba mwanzoni katili mmoja, Anzaruni, aliyeishi kwenye jabali liitwalo “Mlima wa Moshi”, karibu na uwanja wa moto, aliipata na kuimiliki hirizi hii, baada ya kumwua mmiliki wake halali. Mtunzi pia anatueleza kwamba Anzaruni aliiridhi hirizi kutoka kwa mababu wake. Jambazi, kafiri, mnyanganyi, muuaji, mbakaji na mlaaniwa Anzaruni aliwashambulia wapita njia na kuwanyang’anya mali yao na pia kuwanajisi wanawake na kuwaua. Kila aliyejaribu kupigana naye alimshinda. Hatimaye, Mtume Muhammad alipata habari za dhuluma za Anzaruni na, kama ilivyo katika *Utenzi wa Rasil’ghuli, Chuo cha Herekali/Utendi wa Tambuka, Utendi wa Amuri Ghuweni na Utendi wa Katirifu/Wadi Isibani/Seysibani/Waladi Isibani*, akatuma jeshi lake kupigana naye. Vita vikuu vilipiganwa lakini WaIslamu wakashindwa mara nydingi na jeshi kubwa la kafiri Anzaruni. Mtume Muhammad aliendelea kuomba na Mwenyezi Mungu akayajibu maombi yake. Alimweleza kwamba Anzaruni alikuwa akishinda vita kwa sababu alikuwa na hirizi, yenye jina la Allah na iliyo na nguvu za ajabu. Baada ya maombi ya Mtume kujibiwa, kwa malaika Jiburili kutumwa na Allah kumfunulia siri yake. Ndege mweusi aliinyakua hirizi hii kutoka kwa kichwa cha Anzaruni na kumpelekea Ali bin Talib, jagina wa kivita, ambaye alimpatia Mtume Mtume Muhammad. Walipigana tena, lakini wakashindwa, ingawa walikuwa na hirizi hiyo. Mtume Muhammad aliswali tena na mara hii alishauriwa na Allah kuisoma hirizi. Aliampa Sheikh ‘Ali, mkwewe na mojawapo wa masahaba wake sugu, ambaye aliisoma. Malaika elfu sabini waliotumwa kutoka mbingu ya saba walishirikiana na jeshi la Mtume Mumhammad na kupigana hata wakashinda vita, na kumwua katili Anzaruni

Baada ya kupata ushindi vitani, Mtume Muhammad na masahaba wake walirudi kurudi nyumbani, ambako walimkuta mwenzao Abubakari bin Sadiki akiwa mgonjwa. Mtume alipomwekelea Abubakari ile hirizi (Siri ya Siri) alipona

mara moja. Hii ndio sifa ya hirizi – humfaidisha aliyenayo na kuhatarisha maisha ya adui yake. Hirizi hii ilipoingia katika mikono ya WaIslam, waliitumia kumwangamiza jagina Anzaruni (wa Mutiso 2003b, 2010).

Nana Somo (Labda Karne ya 18)

Hatuju mengi kuhusu Nana Somo ila kwamba ni mtunzi wa kike na yumkini aliisihi kabla au katika karne ya karne ya kumi na nane. Yumkini ni mzaliwa na mkazi wa Pate au Lamu. Nana Somo alitunga utenzi maarufu ujulikanano kama *Vita vya Huneni* (Biersteker, 1996:277), utenzi ambao umenakiliwa katika hati ya KiRumi na hayati Mwalimu Pera Ridhiwani, wa Taasisi ya Uchunguzi wa KiSwahili.

Kwa kifupi, mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Hunaini* anasimulia kisa cha mapambano kati ya WaIslam na MaKafiri, huko Uarabuni, wakati wa Mtume Muhamad. Mtunzi wa utenzi huu amefaulu kutusawiria mapisi ya ushindi wa WaIslam, huko Uarabuni katika karne ya saba. Ushindi huu ni ruwaza ya ushindi, matumaini na kichocheo cha mapambano ya WaIslam, dhidi ya wasio WaIslam, hadi leo hii. Mtunzi huyu anatumia mapisi na visakale kuhalalisha na kuendeleza mapambano ya jamii yake ya wakati alioishi Mashujaa wa utenzi huu ni Mtume Muhamadi, jagina Ali bin Abu Twalib, Abubakari na wafuasi wao. Wapinzani wao, ambao mtunzi anawaita “maluuni”, ni Maliki bin Aufi, Said bin Ashirafu, Dhatil Himari na wafuasi wao. Wababe wakuu utamboni ni Shehe Ali, katika upande wa WaIslam, na Dhatil Himari, katika upande wa MaKafiri. Pambano la mwisho kubwa ni kati ya wababe hawa wawili. Katika pambano hili, jagina Ali anamshinda na kumwua Himari. Ushindi huo wa Ali ni ishara ya ushindi wa Uislamu dhidi ya “ukafiri”. Ufundu wa mtunzi unajitokeza katika usimuliasi. Anafaulu kudumisha tataruki au msisimko katika masimulizi yake, kumfanya msomaji ashawishike kuendelea kusoma hadi mwisho wa utenzi. Tazama, kwa mfano, beti zifuatazo (84-91) ambako mtunzi anaonyesha uelewa mkubwa wa hulka ya binadamu mwenye kushikilia lengo lake. Katika beti hizi, Maliki, kiongozi wa MaKafiri, anataka mapambano yaanze lakini anachelea kuwa wenzake watampinga. Kwa sababu hii, anasimulia visa ambavyo vinafafulu kuwashawishi wamuunge mkono. Tukio lingine linalotuongoza kufikia uamuzi kwamba mtunzi anaelewa vyema tabia ya binadamu ni wakati Himari anapopambana na Ali. Mkewe Himari anavua ukaya wake na kumpa mtumwa wake ampelekee Himari na amwambie kuwa asipomuua Ali na kuurejesha huo ukaya ukiwa na damu, basi ajue kuwa hatokubali kukutana naye tena katika nyumba moja (ubeti 772-778). Mtunzi anaitumia vizuri mbinu hii, kama silaha ambayo mkewe Himari anaitumia kumchochea mumewe kupambana kufa kupona.

Binti Said Amin Bin Said ‘Uthman: *Utenzi wa Fatumah* au *Utenzi wa Arusi ya Fatuma na Ali*

Katika 1807, *Utenzi wa Mwana Fatumah* (beti 446) ulitungwa na mtunzi wa kike, ambaye anajiita, Binti Said Amin bin Said ‘Uthman wa ukoo wa Mahadlay /Mahadila/Mahadali. Ukoo wa Mahadali ni mojawqpo ya koo za zamani sana za KiSharifu katika Afrika Mashariki, ukiwemo ukoo wa utawala wa Abu'l Mawahib wa Kilwa, karne ya kumi na tatu, kutoka kusini ya kati ya Yamani. Utenzi huu pia umehusishwa na babake Mwenye Sai'd (Sayyid) Amin wa Sayyid ‘Uthman al-Mahdaly. Yumkini mtunzi ni baba yake Binti Saidi, Said Amin bin Said ‘Uthman/ Sayyid Ahmad bin Hasan al-Mahdali/ Mwenye Said (Sayyid) Amin wa Sayyid 'Uthman al-Mahadaly na Binti Said Amin ni mnukuzi tu. Aidha, inawezekana kwamba Mwenye Said aliutunga akishirikiana na bintiye, kama tutavyooana baadaye, katika maelezo katika mswada mmmoja ulioko SOAS. Huenda hii ni nakala tofauti ya mswada uliotungwa na Mwenye Sai'd. Hakika katika dunia ya miswada, ni vigumu kusema kwa uhakika ni nani mtunzi asilia wa matini. Sehemu ya utenzi huu, ambayo iko katika maktaba ya Chuo cha Dar es Salaam, na ni ya mwaka 1966, ilipatikana kwa Fadhl Muhammad Maawy wa Lamu.

Nakala nyingine yenye beti 446 , na iliyoko katika maktaba hiyohiyo ya Dar es Salaam, ni ya Sheikh Ahmad bin Hasan (mnukuzi?). Muswada huu ulichapishwa na Dammann (1940) katika kitabu chake *Dichtunge In der Lamu mundart des Suaheli Band*. Katika mktaba ya Dar es Salaam, kuna miswada^bifuatayo: Mswada nambari 94B, 98.6, 98.7; 133 (uk. 1-108), 135, 136 (uk. 54-49), 137, 157 (uk.1-63}, 158 (uk.1-22), 169 (uk.38-40 na uk. 167-193), 245, 422 (uk. 59-65), 484 (uk.1-18), 563 (sehemu ya mswada mzima), 574 (uk.31-40), 579 (uk. 5-12) na 809 (uk. 23-44, maelezo). Miswada ambayo nimeirejelea katika kazi hii, nilisoma huko Dar es Salaam na katika SOAS na Ujerumani.

Tarehe kwenye mswada ambao Dammann aliusoma huko Lamu mwaka wa 1973, na alioutumia katika toleo lake ni 1222 A.H au 1807 B.K. (tazama ubeti 444). Dammann anasema:

Nilipata nakala ya shairi hili, ambalo huenda lilitungwa mwaka wa 1936, kutoka kwa Said Ahmed bin Said Pate I-Huseini. Mengine (kuhusiana na shairi hili) sasa hupatikana katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha mji wa Hanse, Hamburg. Mswada huu, haukuandikwa kwa makini sana na yumkini, katika harakati za kuunakilisha, mtunzi wake aliwacha nje beti kadha.

Kulingana na muswada MS 393, faili 279888-Vol.9 na MS 331 faili nambari MS 279888-Vol.5,_katika mkusanyo wa Allen, maktaba ya School of Oriental and African Studies, utenzi huu unaitwa *Utenzi wa Arusi ya Fatuma na Ali/ Utendi wa Arusi ya Fatuma na Ali* na ulitungwa na Sayyid Ahmad bin Hasan al-

Mahdali na kunukuliwa na Maryam binti Ali bin Abdalla na ultungwa katika mwaka wa 1200 A.H/1786 B.K. Katika muswada *Utendi wa Arusi ya Fatuma na Ali*, watanzi ni Sayyid Ahmad bin Hasan al-Mahdali na Amina binti Said Amin na mnukuzi ni Jaylani bin Uthmani al-Amudy na ultungwa 1220 A.H/1805.

Jan Knappert (1979) alitarjumi beti chache za utenzi huu kwa KiIngereza na kuzijadili. Dammann (1940) aliutarjumi utenzi huu na *wa Siri li Isirali* kwa KiJerumani. Nilizitarjumi tenzi hizi mbili na kuzihakikiki kwa KiIngereza na KiSwahili (wa Mutiso2003a, 2003b na 2010).

Utenzi wa Fatuma ni muhimu kwa WaIslamu wote, kwa sababu unahu harusi ya Fatumah, bintiye mtume Muhammad na mkewe Ali bin T(w)alib, jagina wa WaIslamu wote pia. Fatumah ndiye mamake Hassan Hussein, ambao ndio wajukuu wa pekee wa mtume Muhammad. Wazaliwa wa Hassan na Husseini huitwa MaSayyid na MaSharifu. Fatumah ni ruwaza njema na mwenye shufaakwa waawake wote wa KiIslamu. Ndoa yake pia ni ruwaza njema ya ndoa zote za KiIslamu. Tena ndiye mzazi wa vizazi vyote va mtume Muhammd. Maudhui ya utenzi huu yahusu harusi ya Fatumah na Ali bin T(w)alib. Aidha unahu kuumbwa kwa dunia, sifa za Mwenyezi Mungu, mtume Muhammad, Ali bin Abii T(w)alib na malaika.

Marejeleo

- Abdulaziz, M. H. (mhar./mtarj.). (1979). *Muyaka: 19th Centuary Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Allen, J. W.T. (mhar./mtarj.) (1971). *Tendi-Six Examples of Swahili Classical Verse*. Nairobi: Heinemann Ltd
- Allen, J. V. (1993). *Swahili Origins: Swahili Culture & the Shungwaya*. London: East African Educational Publishers.
- Allen, J. V. & Wilson, T. H. (Mhr.) (1979). "Swahili Houses and Tombs of the Coast of Swahili Coast of Kenya", London: Art and Archaeology Research Papers.
- Allibert, C. (2000). "La chronique d'Anjouan par Said Ahmed Zaki (ancient cadi d'Anjouan)." *Études océan Indien* 29:9–92.
- Amirell, S. (2015). "Female Rule in the Indian Ocean World (1300-1900)". *Journal of world history* 26(3): 443-489
- Askew, K. M. (1999). "Female Circles and Male Lines: Gender Dynamics along the Swahili Coast." *Africa Today* 46: 3–4, 67–102.
- Bennett, N. R. (1978). *A History of the Arab State of Zanzibar*. London: Methuen & Co Ltd.
- Berg, F. J. (1968). "The Swahili community of Mombasa 1500-1900", *Journal of African History* 9 (1): 35-56.
- Biersteker, A. (1991). "Language, Poetry, and Power: A Reconsideration of *Utendi wa Mwana Kupona*", *Faces of Islam in African Literature* 59-77.
- _____ (1996). *Kujibizana*. East Lansing: Michigan State University Press

- Boxer, C.R (1952). "A glimpse of the Goa Archives", Bulletin of the School of Oriental and African Studies XIV/2: 299-325
- Brown, M. (1995). *A History of Madagascar*. Damien Tunnacliffe.
- Chiraghdin, S. (mhar.) (1975). "Utangulizi wa Mhariri", katika Ahmad Nassir Juma Bhalo, *Malenga wa Mvita* 5-6.
- Chiraghdin, S & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Damir, B. A n.w (1985). *Traditions d'une lingée royale des Comores*. Paris: l'Harmattan.
- Dammann, Peter Ernest (1940). *Dichtungen in der Lamu Mundart des Suaheli* 28. Hamburg: reiderichesen
- Elliot, J. A. G (1925-26). "A Visit to the Bajun Islands: Part I & II". *Journal of the Royal African Society* 25 (99): 10-22, 147-163, 245- 263, 338-358
- Freeman, G. (1962/1975). *The East African Coast: Select Documents from the First to the Earlier Nineteenth century*. Oxford: Clarendon Press/Rex Collings.
- Freeman, G. & Martin, B. G. (1973). "A Preliminary Handlist of the Arabic Inscriptions of the Eastern African Coast". *Journal of the Royal Asiatic Society of Great Britain and Ireland* (2):98-122
- Gower, R. n.w. (1996). "Swahili Women Since the Nineteenth Century: Theoretical and Empirical Considerations on Gender and Identity Construction". *Africa Today* 43 (3): 251-268
- Gray, J. M. (1952). "A History of Kilwa: Part II". *Tanganyika Notes and Records* 32:11-37.
- _____ (1960). "Zanzibar Local Histories, Part I". *Swahili* 30:24-50.
- _____ (1961). "Zanzibar Local Histories, Part II". *Swahili* 31:111-139.
- _____ (1962). *History of Zanzibar from the Middle Ages to 1856*. London: Oxford University Press.
- _____ (1977). "The Hadimu and Tumbatu of Zanzibar", *Tanzania Notes and Records* 81 (82): 135-153
- Harris, L. (mtarj/mhar) (1938). "Khabar al Lamu-A chronicle of Lamu" (mtunzi ni Shaibu Faraji b. Hameda l-Bakari al-Lamuy), *Bantu Studies* 12 (1):1-33
- _____ (1959). "Swahili Traditions of Mombasa", *Afrika und Übersee*, Band 73: 81-105.
- _____ (1962). *Swahili Poetry*. London: Oxford University Press
- _____ (1977). *The Swahili chronicle of Ngazija* (mtunzi ni Said Bakari bin Sultan Ahmed). Bloomington: African Studies Program Indiana University Press
- Hichens, W. (mhar.) (1938a). "Diwani ya Malenga wa Sawahili: Anthology of Swahili Poets: The Azanian Classics IV" (muswada ambao haujachapishwa bado), SOAS, London
- _____ (1938b). "Khabar al-Lamu-A Lamu Chronicle" (kilichotungwa na Shaibu Faraji bin Hamed Al-Bakariy Al-Lamuy), *Bantu Studies* 12: 1-33

- Ibn Battūṭa. 1994. (1355). *The Travels of Ibn Battūṭa A.D. 1325–1354* vol. 4, (mhar.) H. A. R. Gibb. London: The Hakluyt Society
- Ingrams, W. H. (1931/1967). *Zanzibar: Its History and Its People*. Inter-Territorial Language Committee for the East African Dependencies, under the direction of the late Frederick Johnson London: H. F. & G. Witherby
- Khatib, M.S. (1985). “Utensi wa Mwanakupana”. *Mulika*, 17: 46-52
_____. (1962/63). “Swahili Prosody”. *Swahili* 33 (1): 107-137
- Kirkman, J. S. (?) “The Jumma of the Three Tribes at Mombasa: A Swahili osque”(Ripoti ya mapisichimbo ambayo haijachipishwa bado na iko katika Maktaba ya Makumbusho ya Ngome ya Isa”): 8-9.
- Knappert, J. (1964a). *Four Swahili Epics*. Leiden: Drukkerij” Luctor et Emergo
_____. (1964b). “Asili ya Mvita”. *Swahili* 34/2:21-24
_____. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. Leiden: E. J. Brill
- Maawy, A. A. A. (2011). *Jawabu la Mwana Kupona*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam
- Mathew, G. (1956). “The Culture of the East African Coast: In the Seventeenth and Eighteenth Centuries in the Light of Recent Archaeological Discoveries”, *Man* 56: 65-68
- Molet-Sauvaget, Anne (mhar.) (1994). *Documents anciens sur les îles Comores(1591–1810)*. Paris: Institut des Langues et Civilisations Orientales
- Morris, E.G & Snoxall, R. A. (1965). *Elimu ya Kiswahili: Kitabu cha Pili*, Arusha: Longman of Tanzania Limited
- Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu*. Dar-es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mulokozi, M. M. & Sengo, T.Y. (1995). *History of Kiswahili Poetry A.D 1000 -2000*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research
- Nicholls, C.S. (1971). *The Swahili Coast: Politics, Diplomacy and Trade on the East Littoral 1798-1856* 2. London: George Allen & Unwin.
- Njozi, H. M. (1990). “Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetic”. *Kiswahili* 57: 55-67.
_____. (1993). “The Social Context of Utendi wa Mwanakupona”. *Frankfurter Afrikanistische Blätter* 5: 83-90.
- Nurse, D. & Spear, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the History and Languages of an African Society, 800-1500*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Omar, Y. A. & Frankl, P. J. L. (1994). “A 12th/16th century Swahili letter from Kilwa Kisiwani”(being a study of one folio from the Goa Archives), *Afrika und Übersee* 77: 263-272
_____. (2000). “Siku ya Mwaka: The New year (with special reference to Mombasa)”, Swahili Forum VII: 5-31
- Piggott, D.W.I. (1941). “History of Mafia”. *Tanganyika Notes and Records* 11: 35-40

- Pouwels, R. L. (1971). *Origins of Arabic Settlement of East Africa to the Tenth Century*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Duquesne.
- _____. (1979). *Islam and Islamic Leadership in the Coastal Communities of Eastern Africa, 1700-1914*, Los Angeles: Tasmifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha California.
- _____. (1984). "Oral Historiography and the Shirazi of the East African Coast", *History in Africa* 11: 237-267
- _____. (1987). *Horn and Crescent: Cultural Change and Traditional Islam on the East African Coast, 800-1900*. Cambridge: Cambridge University Press,
- Prins, A. H. J. (1961/1967). *The Swahili-speaking Peoples of Zanzibar and the East African Coast*, London: International African Institute
- Saadi, K. A. O. (1941). "Mafia History and Traditions", *Tanganyika Notes and Records* 1 2:23-27.
- Sacleux, C. (1891/1959). *Dictionnaire Français-Swahili*. Paris: Institut d'Ethnologie.
- Shepherd, G. (1977)."Two Marriage Forms in the Comoro Islands: An Investigation", *Africa* 47 (4):344- 358.
- Shariff, I. N. (1987). *The Function of Dialogue Poetry in Swahili Society*. New Brunswick: Rutgers The State University of New Jersey
- Stewart, J. (1999). *African States and Rulers*. Jefferson, N.C.: McFarland.
- Stigand, C. H. (1913/1966). *The Land of the Zanj: Being an Account of British East Africa, its Ancient History and Present Inhabitants*. London: Constable and Company Ltd
- Strandes, J. (1961). *The Portuguese Period in East Africa* (Kimetaarjumiwa kwa Kiingereza na Jean F.Wallwork). Nairobi: East African Literature Bureau.
- Strobel, S. (1975). "Women's Wedding Celebrations in Mombasa, Kenya". *African Studies Review* 18 (3):35-45.
- _____. (1979). *Muslim Women in Mombasa, 1890-1975*. New Haven: Yale University Press.
- Taylor, W. E. (1924). *African Aphorisms or Sawas from Swahili-land*. London: The Sheldon Press
- Tolmacheva, M. (mhar/mtarj.) (1993). *The Pate Chronicle*, East Lansing: Michigan State University Press.
- Trimingham, J. S. P. (1964). *Islam in East Africa*. Oxford: Clarendon Press.
- Truhart, P. (2002). *Regents of Nations: Systematic Chronology of States and Their Political Representatives in Past and Present: A Biographical Reference Book. Part 2: America and Africa*.
- wa Mutiso, K. (2014a). "Number Symbolism (nos.1, 4, 7 and 1,000) in Swahili Poetry: The case of *Utenzi wa Fatumah*", *Kiswahili* 77: 132-148
- Walter, B. J. (1968). "Mosques, Population and urban Development in Mombasa", *Hadith* 1: 47-100.
- _____. (2014b). "Number Symbolism in World Religions: The Case of Number Seven", *Journal of Oriental and African Studies* 23: 405-415
- _____. (2014c). "Sexism in Forbidden Language: The case of Kiswahili and

- English”, *Journal of Oriental and African Studies* 23: 353-379
- _____ (2012) “Motifu ya Hirizi katika Ushairi wa Kiislamu wa Kiswahili”. *Mulika* 31:115-135.
- _____ (2010). *Five Swahili Epics by Four Swahili Women: Utensi wa Siri li Asirali, Fatumah, Mwana Kupona, Howani Mwana Howani and Mwanakukuwa* (muswada ambao haujachapishwa bado)
- _____ (2005). *Utenzi wa Hamziyyah*. Dar-es-Salaam, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam
- _____ (2003a). “Number Symbolism in Swahili Epics” (makala ambayo hayajachapishwa bado), niliyawasilisha tarehe 13 Februari, 2003, Institut Fur Afrikanistik, Koln: Univesität Koln
- _____ (2003b). *Utenzi wa Siri li Asirali* (The Secret of the Secrets, mswada), tarjumi ya kwanza na maelezo kwa Kiingereza
- _____ (2003c). *Utenzi wa Mwanakupona* (Mwanakupona Epic, mswada), tarjumi na maelezo kwa Kiingereza
- _____ (2002). *Utenzi wa Fatumah* (Mwana Fatumah Epic, mswada), tarjumi ya kwanza na maelezo kwa Kiingereza
- _____ (1985a) .*Hurafa na Uyakinifu katika Hamziyyah*, Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi
- _____ (1985b). *Kasida ya Hamziyahab*, Tarjumi ya kwanza ya Kiingereza pamoja na maelezo kwa Kiingereza (mswada)
- Werner, A. (1914). “Some Notes on East African Folklore Some Notes on East African Folklore”, *Folklore*, Vol. 25, No. 4 (Dec. 31): 457-475
- _____ (1914/5). “A Swahili History of Pate”, *Journal of the Royal African Society* 14: 148-161; 278-297; 392-413.
- Werner, A. & Hichens, W. (1937). *The Advice to Mwana Kupona upon Wifely Duty*. Medstead Medstead: The Azania Press.
- Ylvisaker, Marguerite H (1979). *Lamu in the Nineteenth Century: Land, Trade and Politics*. Boston: African Studies Centre, Boston University.